

Ukweli Hauna Kutu

Pambazuko

Toleo Namba 018

Jumatatu Novemba 7-13, 2022

CAG, Bunge na kazi ya Panado Uk. 4



Huzuni

- Simulizi ya shuhuda yasikitisha
- Wavuvi waoko a 26 ajali ya ndege
- Majaliwa kuaga miili kitaifa leo
- Pata majina ya manusura, waliofariki

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Wapongezwe wavuvi kwa kuokoa maisha


MENGI yanaweza kusemwa na wanasiasa na kupongeza wasiokuwa wahusika wakuu wa uokozi katika ajali ya ndege ya Shirika la Ndege la Precision, iliyolazimika kutua ndani ya maji ya Ziwa Victoria jirani na Uwanja wa Ndege wa Bukoba, Kagera.

Lakini ukweli lazima usemwe, waokozi wakuu walikuwa ni wavuvi, wakisaidiwa na wanajeshi wachache sana wenye ujuzi wa kuyamudu na kuyakabili maji.

Sisi katika Pambazuko, tunawapa kongole wavuvi zaidi, kwa kuwa tumeshuhudia kilichokuwa kikiendelea katika juhudi za kuokoa abiria na wahudumu wa ndege ya Precision iliyopata ajali asubuhi ya Novemba 6, 2022.

Hongereni sana wavuvi ndani ya Ziwa Victoria, eneo la Bukoba. Mnastahili kupewa nishani kwa juhudi zenu hata kama juhudi hizo zilikoma baada ya wanasiasa kufika eneo la tukio na kutoa “uamuzi” wao kuhusu zoezi la kuokoa.

Tutoe pongezi panapostahili.



Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: pambazuko1@protonmail.com ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



“Haki ni tunu kuu kulinda uhai wa taasisi za kijamii kama ambavyo ukweli ni tunu ya kwanza kutunza heshima kisayansi. Hata kama nadharia ya kisayansi ni maarufu kiasi gani, inapaswa kutupiliwa mbali kama ukweli wake umechuja. Ni vivyo hivyo, kwa taasisi za kijamii, bila kujali zinaleta ufanisi kiasi gani, zinapaswa kurekebisha au kubomolewa kama zimepoteza sifa ya kutenda haki.” - Profesa John Rawls, 1971

Mungu asiingizwe kwenye katiba mpya**Pepricles Mayombo**

TANZANIA ni taifa linalojumuisha wachamungu, wakanamungu na washukumungu. Yaani, “theists, atheists and agnostics.” Hivyo, najenga hoja kupinga neno “Mungu” kupenyezwa kwenye katiba Mpya.

Wachamungu (theists) wanabeba hoja ifuatayo: Imani kwamba Mungu yupo inaungwa mkono na ushahidi mkubwa; endapo Imani kwamba kitu kipo inaungwa mkono na ushahidi wa kutosha, inabidi kukubali madai kwamba kitu hicho kipo; Hivyo, inabidi kukubaki kwamba Mungu yupo.

Wakanamungu (atheists) wanabeba hoja ifuatayo; imani kwamba Mungu yupo inaungwa mkono na ushahidi mdogo; endapo imani kwamba kitu kipo inaungwa mkono na ushahidi hafifu, inabidi kukataa madai kwamba kitu hicho kipo; Hivyo, inabidi kukataa madai kwamba Mungu yupo.

Na washukumungu (agnostics) wanabeba hoja ifuatayo; imani kwamba Mungu yupo inaungwa mkono na ushahidi mdogo; endapo imani kwamba kitu kipo inaungwa mkono na ushahidi hafifu, inabidi kujiuziai kukubali au kukataa madai kwamba kitu hicho kipo; hivyo, inabidi kujizuia kukubali au kukataa madai kwamba Mungu yupo.

Maneno “ushahidi mkubwa” na “ushahidi mdogo” maana yake ni rahisi kuielewa. Kila mtu anayekubali sentensi kama vile, “Mungu yupo,” hapo hapo anakuwa amezikataa sentensi mbili zingine kwa mpigo. Sentensi ya pili inayokuwa imekataliwa ni, “Mungu hayupo.” Na sentensi ya tatu inakuwa imekataliwa ni, “ama Mungu yupo au Mungu hayupo.”

Endapo angalau asilimia 51 ya ushahidi ulio kwenye kapu la ushahidi inaunga mkono kauli kwamba “Mungu yupo,” basi sentensi mbili baki zinahesabiwa kwamba sio kweli.

Endapo angalau asilimia 51 ya ushahidi ulio kwenye kapu la ushahidi inaunga



mkono kauli kwamba “Mungu hayupo,” basi sentensi mbili baki zinahesabiwa kwamba sio kweli.

Na endapo asilimia 50 ya ushahidi ulio kwenye kapu la ushahidi inaunga mkono kauli kwamba “Mungu yupo,” na asilimia 50 ya ushahidi uliobaki inaunga mkono kauli kwamba “Mungu hayupo,” basi, hapo hakuna kambi iliyoshinda.

Badala yake, tunabaki tumesimama mguu pande kwa kusema kuwa, “ama Mungu yupo au Mungu hayupo,” mpaka hapo ushahidi wa kupiku upande mmoja utakapopatikana.

Kwa sababu hii, ni sahihi kusema kuwa, hakuna seti ndogo ambayo ni mwafaka kati ya kambi tatu za wachamungu, wakanamungu, na washukumungu.

Hata kambi ya wachamungu inagawanyika katika makundi kadhaa, pale swali “Mungu anazo sifa zipi?” linapoulizwa. Baadhi watasema anazo nafsi tatu, wengine watakataa; baadhi watasema anaruhusu ndoa za mitala, wengine watakataa; baadhi watasema anaruhusu kondomu, wengine watakataa, wengine watasema anaruhusu kitimoto, wengine watakataa; na orodha inaendelea.

Kwa hiyo, madai kwamba kama neno “Mungu” litaingizwa kwenye Katiba ya nchi litakuwa alama ya umoja wa kitaifa, hayasemi ukweli wote. Hivyo, napendekeza kuwa neno “Mungu” lisingizwe katika Katiba Mpya ya Tanzania.

CAG, Bunge na kazi ya Panado

Na Dkt. Bullet RUHINDA

WENGI wetu tukipata maumivu ya kichwa au sehemu nyingine ya mwili, hukimbilia kumeza dawa ya maumivu maarufu kama Panado au Aspirin.

Lakini wengi tunajua kwamba dawa ya maumivu haiponyi, bali inafubaza maumivu kwa muda, wataalamu wanasema inausahulisha ubongo kwamba kuna maumivu sehemu fulani mpaka hapo itakapopatikana tiba. Kwa hiyo, hatuwezi kupona maumivu ya kichwa kwa kumeza Panado ambayo husitisha maumivu kwa muda.

Watanzania wengi ni masikini. Sababu za umasikini ni nyingi na siyo rahisi kuzitaja zote. Masikini kawaida anatakiwa kutumia mali zake kwa uangalifu sana.

Katika nchi yetu ili kujua kama mali zetu hasa rasilimali fedha inatumika kwa kadri ya umasikini wetu, katiba ilitupatia Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Kila mwaka anafanya kazi yake kwa kadri awezavyo. Mara nyingi sana taarifa yake inaibua madudu mengi ya ubadhirifu wa mali ya umma.

Kwa akili za kawaida tunategemea kwamba serikali itayafanya kazi mapendekezo ya CAG ili kuondoa ubadhirifu huo. Isiyokuwa bahati, badala ya kuukomesha ubadhirifu na wizi unaoibuliwa na ofisi ya mkaguzi, kumekuwepo na kitu kinachofanana na kuahirishwa kwa matatizo hayo mpaka taarifa ya mwaka unaofuata, hivyo wananchi kusahau taarifa ya mwaka husika.

Serikali badala ya kututafutia dawa, inatupatia dawa ya kufubaza maumivu, yaani Panado kwa kuleta taarifa bungeni ambapo wabunge hujadili kwa ukali sana na hivyo kutuamianisha kwamba itafanyiwa kazi.

Kwa maneno mengine, bunge ni Panado yetu ya kutusahulisha maumivu yaliyosababishwa na taarifa ya CAG mpaka mwaka unaofuata tutakapopata



CAG Charles Kichere

maumivu mapya baada ya ripoti mpya kusomwa.

Hebu katika hali halisi tuchukue mifano miwili ya ubadhirifu uliojadiliwa bungeni kutokana na taarifa ya CAG tuone ni kwa kiasi gani itafanyiwa kazi. Tuone kama kuna mtu au watu watawajibika au kuwajibishwa kwa kadhia hizo.

Mfano wa kwanza ni ile nukuu ya Mbunge wa Sengerema, Tabasamu Hamisi Hussein Mwangao kwamba mamilioni ya dola yaliyotokana na malipo ya visa katika ubalizi wetu Marekani yameibwa. Mfano wa pili ni kuwepo kwa wilaya moja yenye ofisa mmoja aliyechepusha mamilioni ya shilingi yaliyotolewa na Kampuni ya Umeme Tanzania (Tanesco) kulipa fidia na kutengwa kwa kiasi cha kumpatia mkuu wa wilaya milioni tisini ili kumyamazisha (yeye alitumia maneno “kumkata ngebe”).

Je, kuna balozi au waziri atawajibika kwa suala la upotewe wa mamilioni ya dola za visa? Je, hizo pesa za Tanesco zitaondoka na mtu? – maana hiyo ndio dawa ya ugonjwa au tutaendelea kupata Panado na kazi iendeleo?

Tutafakari.

Matukio mbalimbali ya ajali ya ndege ya Precision



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akimpa pole Edwin Bitegeko ambaye amenusurika katika ajali ya ndege ya Precision iliyotokea jana mjini Bukoba. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)



Matukio mbalimbali ya ajali ya ndege ya Precision



Mkuu wa mkoa wa Kagera Albert Chalamila akiwa katika eneo ajali jana mjini Bukoba



Nguzo ya demokrasia - II

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

NILIELEZA kuwa ningetaja nguzo saba za demokrasia na katika toleo lililopita nilitaja mbili, hivyo leo nitazungumzia moja kati ya zile tano zilizobaki.

Tatu, ushiriki wa watu katika uendeshaji wa taifa lao. Ni vyema tuendelee kukumbuka kwamba utawala wa demokrasia ni utawala wa watu. Watu hao ndio hutoa ridhaa ya kuweka miundo na mifumo ya jinsi ya kuendesha taifa lao ikiwemo kutoa ridhaa kwa baadhi ya watu na makundi kufanya hivyo kwa misingi ya sheria walizozitunga kama miongozo ya kufuatwa.

Sheria hapa ni katiba na sheria zote zinazofafanua yale yaliyomo kwenye katiba hiyo ambayo ni sheria mama. Kwa hiyo ni watu hao ndio huamua ni kiasi gani cha madaraka kitolewe kwa nani, kwa malengo gani na kwa muda gani.

Suala la upimaji wa kiasi cha madaraka na nguvu na uratibishwaji wake, ni sawa na kauli ya ridhaa ya watu wenyewe, hivyo ni lazima iwemo katika sheria hizo. Na kwa kusema hivyo, maana yake ni kwamba ni lazima wanaozitunga sheria hizo wawe ni wananchi wenyewe kwa uhuru wao na kwa njia ya taratibu walizoridhia zitumike.

Kukasimia madaraka kwa watawala siyo kujitoa kwa watu katika kutawala. Ikumbukwe kwamba kwa kawaida wale wanaopambana kuingia madarakani wana uchu wa madaraka.

Inawezekana wakatofautiana viwango vya uchu huo, lakini kwa jumla wote wana kiwango fulani cha uchu huo. Na hii siisemi hapa kwa maana mbaya, kwani uchu huo pia ni kipawa kizuri japo walio wengi wana uchu mbaya wa madaraka.

Ni hatari kumpa uongozi mtu asiyekuwa na hamu ya kuongoza kama ilivyo hatari kumpa madaraka mtu aliye na uchu muovu wa madaraka. Kwa sababu ya hulka za jinsi hiyo, ni muhimu



uwepo ushiriki wa watu wenyewe katika hatua na vipindi mbalimbali vya watawala ili kuzuia nia ovu ya watu wenye uchu mbaya kupokonya nguvu ya umma.

Ili kudhibiti hilo ndio sababu ni muhimu sheria ziweke wazi suala la uratibishwaji wa madaraka hayo. Hata hivyo, pamoja na kuweka sheria lakini tukumbuke kwamba sheria hushughulikia makosa yaliyotendeka na hujengwa katika uzoefu wa mapungufu hayo.

Kwa kutambua upungufu wa sheria na kwa kujua hulka ya watu ya “uchu mbaya wa madaraka” unaoweza kutumbukiza taifa katika utawala wa kidikteta, ndipo hujitokeza umuhimu wa ushiriki wa umma katika utawala wa taifa lao.

Hii ni pamoja na kuwa na taratibu huru za kutoa maoni na kuhoji juu ya mambo mbalimbali. Taratibu kama hizo haziasilishwi na wale walioko madarakani bali kwa mujibu wa sheria huru zilizotungwa kwa uhuru wa wananchi.



Elon na ukanganyifu wa Twitter

TUNAISHI katika zama ambapo mtandao wa kompyuta – intaneti – unazidi kuwa kama miongoni mwa mahitaji muhimu ya mwanadamu (basic human needs).

Na moja ya maeneo ya intaneti yanayotumiwa zaidi na wanadamu ulimwenguni kote ni katika mitandao ya kijamii.

Miongoni mwa mitandao hiyo ya kijamii ni Twitter, ambayo hivi majuzi imepata mmiliki mpya, mtu tajiri kuliko wote, Elon Musk.

Hata hivyo, mchakato uliosababisha Elon kuwa mmiliki wa Twitter uliambatana na changamoto mbalimbali.

Kwanza, mara baada ya tajiri huyo kutangaza nia ya kununua Twitter, watumiaji mbalimbali wa mtandao huo wa kijamii, hususan wa mrengo wa kiliberali walionyesha shaka yao.

Kabla ya kununua mtandao huo wa kijamii, Elon, mmoja wa watumiaji wa Twitter wenye mamilioni ya wafuasi (followers), alionekana bayana kuelekea - siyo tu upande wa wenye itikadi za kihafidhina, bali pia upande wa makundi yenye msimamo mkali dhidi ya uliberali.

Makundi haya ni pamoja na wabaguzi wa rangi (racists), wanaonyanyapaa wanawake (misogynists), wapinzani wa uanamke (incels), manazi, na makundi mengine unayoweza kutamka bila shaka kuwa yanafanya mitandao ya kijamii kuwa sehemu hatari.

Elon alionekana kuelekea upande huo kwa kutumia bango la uhuru wa kujieleza (freedom of speech). Kwamba, wabaguzi wa rangi wana haki ya kusema chochote kile hata kama kinakiuka haki za watu wengine.

Kwamba wanyanyasaji na wanyanyapaaji wa wanawake wana haki ya kutoa maoni yao kama ilivyokuwa kwa makundi mengine.



Elon Musk.

Hata hivyo, alifanikiwa kuinunua Twitter, na baadaye Elon alijigamba kwamba “ndege sasa yupo huru” (ndege ni nembo ya Twitter) akimaanisha kuwa kila mtu atakuwa na uhuru wa kusema chochote kile. Lakini pia anapaswa kuelewa kwamba haki ya kusema chochote shurti iendane na wajibu wa kuheshimu haki za wengine.

Takriban wiki baada ya Elon kuwa mmiliki wa mtandao huo wa kijamii, mambo yanaelekea kwenda mrama. Baadhi ya kampuni zimesitisha kuweka matangazo yao Twitter (chanzo kikuu cha mapato kwa mitandao ya kijamii ni matangazo) yakihofia kuwa msimamo wa Elon kuhusu “uhuru kwa kila mtu” unaweza kuifanya Twitter isiwe sehemu salama.

Mwisho, ni mapema mno kumhukumu Elon, lakini yayumkinika kuhisi kuwa anakabiliwa na mthiani mkubwa kuifanya Twitter, siyo tu iendelee kutumiwa na watu wengi, bali iwe na ufanisi zaidi ya ilivyokuwa awali na iendelee kuaminika.

Makala hii ni endelevu.

Wavuvi waokoa 26 ajali ya ndege

**Na Mwandishi WETU
Bukoba**

WATANZANIA 18 na Mwingereza mmoja, jana walishindwa kuingia mjini Bukoba, wakiwa hai baada ya maisha yao kukatizwa na ajali ya ndege iliyowatoa Dar es Salaam wakiwa salama.

Hawa ni miongoni mwa abiria 43 walioelezwa kuwamo ndani ya ndege aina ya ATR42-500 mali ya Shirika la Precision iliyolazimika kutua ndani ya Ziwa Victoria, mita 150 kutoka Uwanja wa Ndege wa Bukoba.

Ndege hiyo yenye usajili 5H-PWF namba PW 494 iliyoanza safari yake kuelekea Bukoba alfajiri ya Jumapili, Novemba 6, mwaka huu, iliingia anga la mji huo pembezoni mwa Ziwa Victoria, lakini rubani wake, Buruani Rubaga alishindwa kutua uwanjani kutokana na hali ya hewa kuwa mbaya.

Mashuhuda waliokuwamo ndani ya ndege hiyo wamelieleza Pambazuko kuwa Rubani Rubaga, akisaidiwa na rubani msaidizi, Peter Odhiambo, alilazimika kuwatangazia abiria kwamba hataweza kutua uwanjani hapo kwa kuwa hali ya hewa kuwa mbaya.

Anga la Bukoba – hasa eneo la uwanja wa ndege jana lilionekana kugubikwa na kungu na mvua iliyokuwa ikiendelea kunyesha tangu alfajiri ya siku hiyo.

Hata hivyo, baadaye rubani hiyo, inaelezwa aliamua kutumia uzoefu wake kutaka kutua uwanjani hapo kupitia eneo la Nshambya ambapo kulikuwa na upepo mkali, hali iliyosababisha kushindwa kuimudu na hatimaye kutua majini. Kawaida, ndege hiyo hutua kupitia eneo la Musira ambalo kwa jana lilikuwa na hali mbaya ya hewa – kutanda kwa ukungu mzito.

Baada ya ndege hiyo kulazimika kutua majini, saa 2.53 asubuhi, wavuvi waliokuwa ziwani, ndiyo walikuwa wa kwanza kufika eneo ilipotua ndege hiyo,

ikiwa imezama sehemu kubwa ya mbele na kubakiza eneo la nyuma likionekana juu ya maji. Ndege hiyo ilitarajiwa kutua saa 2.30 asubuhi na kuondoka kurejea Dar es Salaam kupitia Mwanza saa 2.50 asubuhi.

Mmoja wa waandishi wa Pambazuko aliyekuwapo uwanjani hapo, alishuhudia maji mengi yakiruka, mfano wa wimbi kubwa la maji, kabla ya kubaini kuwa ni ndege aliyotarajia kupanda kurejea Dar es Salaam, ndiyo imetua ziwani.

Shughuli za uokozi zaanza

Baaada ya “kishindo” hicho ndani ya maji, takribani dakika 27, gari la Zimamoto lililokuwa uwanjani hapo lilionekana likiondoka mahali linapoegeshwa huku likiwasha vimwekamweka na likipiga king’ora na ndipo kuwashtua wafanyakazi uwanjani hapo “waliovamia” uwanja na kuanza kulia kwa kelele.

Pambazuko liliwashuhudia wafanyakazi hao wakipiga yowe na kulia na ndipo idadi kubwa ya watumishi wa uwanja huo walipoungana nao kukimbia wakielekea eneo la tukio.

Ndege hiyo ya abiria ilitua ndani ya ziwa hilo, mita takribani 180 kutoka kwenye barabara ya kutua.

Baadaye idadi ya wavuvi iliongezeka huku ndege ikiwa imezima na ghafila, saa 3.11 asubuhi, mlango wa nyuma wa ndege ulifunguka na wavuvi waliokuwa jirani waliingia ndani ya ndege hiyo kuanza uokozi.

Dakika 13 baadaye, askari wa Zimamoto na mwanajeshi mmoja aliyetajwa kuwa mtumishi wa uwanja huo, mwenye uzoefu wa kuogelea, aliingia ndani ya ndege hiyo na kuongeza kasi ya kuokoa idadi ya watu waliokuwa wakisukumwa kutoka ndani ya ndege hiyo.

Pambazuko lilishuhudia wanajeshi wachache na mgambo wakiingia uwanjani hapo saa 3.27 wakikimbia

Wavuvi waokoa 26 ajali ya ndege

Inatoka Uk. 10



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza na wananchi baada ya kuwasili mkoani Kagera, Bukoba kufuatia ajali ya ndege ya Precision Air iliyotokea leo Novemba 06, 2022 mjini Bukoba (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

kuelekea ukingoni mwa ziwa kwa ajili ya kuongeza nguvu za kuokoa, hata hivyo, hawa hakuna aliyekwea mtumbwi ili kwenda kuingia ndani ya ndege kusaidia uokozi.

Hawa walifika wakiwa na mavazi yao ya kazi, magwanda bila vifaa vya uokozi ndani ya maji. Hata hivyo, baadaye ilikuja timu ya wanajeshi wakiwa na vifaa vya kuogolea na kwenda kuongeza kasi ya kutoa abiria ndani ya ndege hiyo wakisaidiana na wavuvi.

Kazi ya kuokoa yasitishwa

Ilipofika saa 5.21 asubuhi, wanajeshi wachache na wavuvi waliokuwamo ndani ya ndege wakipambana kuokoa maisha, walioanza kutoka ndani, huku nyuso zao zikionekana kukata tamaa na 'kuvaa' sura zenye huzuni.

Mmoja wao amezungumza na Pambazuko na kueleza kwamba walilazimika kutoka ndani kwa kuwa maji yaliongezeka, hivyo kuhofia madhara zaidi na wao kujinusuru kwa kuwa abiria kadhaa waliwaona wamefariki dunia tayari.

“Maji yaliongezeka, waokozi wengi tulikuwa tunatembea wakati maji yalikuwa viunoni, lakini baadaye yakafika

vifuani, na hapo tukaona heri kupambana kuokoa tukiwa nje ya ndege maana kubaki ndani kungeweza kuleta maafa zaidi,” ameliambia Pambazuko mmoja wa waokoaji aliyekataa kutajwa jina.

Shuhuda huyo na mwokozi wa abiria anaeleza kuwa ndani ya ndege, abiria waliokuwa wamefariki walikutwa wamefunga mikanda, huku wengi wakiwa wanavuja damu kwenye mapaji ya uso.

“Inaonekana abiria wengi walipata majeraha vichwani na wengine kubainika wamevunjika shingo, hawa tulioona wamefariki, tuliwaacha kwanza na kupambana na wale waliokuwa wakipumua,” anaongeza muokoaji mwingine, Geoffrey Mshemwa.

Aokolewa na kukimbia

Abiria mmoja, miongoni mwa hao 26 waliookolewa, alikimbia mara baada ya kufikishwa nchi kavu na hakuweza kukamatwa, licha ya kufuatiliwa na wana usalama wa uwanja huo.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa abiria huyo mwanaume, huenda alichanganyikiwa na asijue alilokuwa akilifanya kutokana na mshtuko wa ajali hiyo.

Wavuvi waokoa 26 ajali ya ndege

Shuhuda mwingine anena

Mmoja wa mashuhuda aliyekubali kutajwa jina lake ni Richard Komba, ambaye aliliambia Pambazuko kwamba ndege waliyopada iliondoka Dar es Salaam saa 6.15 alfajiri jana, ikiwa ni dakika 15 kuchelewa kuliko ilivyopangwa.

Amesema kuwa safari yao ya kwenda Mwanza kupitia Bukoba haikuwa na msukusuko angani, lakini baadaye walihisi kuwepo kwa hali mbaya ya hewa walipokuwa wakikaribia Bukoba kwani ndege ilionekana kuyumba na kusokwasokwa na nguvu ya upepo.

“Tulipokaribia uwanja wa ndege wa Bukoba rubani alitufahamisha kuwa ameshindwa kutua na alikuwa anaendelea kuona uwezekana wa kutua salama ama kuelekea Mwanza kwanza, lakini inaonekana alishindwa kumudu hali ya hewa na ghafla tukajikuta tumetumbukia majini,” amesema.

Komba amesema mara baada ya kutua kwa kishindo majini, abiria walionekana kuchanganyikiwa, baadhi wakiwa wanapiga kelele na wengine wakionekana kupambana kutafuta mahali pa kujiokoa na ghafla mlango wa nyuma ulifunguliwa na ndipo hekaheka za kujiokoa zikashika kasi, na muda mfupi baadaye aliona watu wakiingia kuwaokoa.

Waliookolewa watajwa

Majina ya watu waliookolewa yametajwa na kwamba wengi walipelekwa hospitali ya mkoa kwa ajili ya uchunguzi zaidi. Wapo walioruhusiwa kuondoka jana jioni na wengine kubaki kwa ajili ya uangalizi zaidi.

Hawa ni pamoja na Ragi Samwel Inyoma (28) mkazi wa Dar es Salaam, Rausath Hassan (26) mkazi wa Bukoba, Anna May Mitabalo (40) mkazi wa wilaya ya Karagwe, Kagera, Dkt. Felix Otieno (37) mkazi wa Bunda, Mara, Shamiru Ismail (34) mkazi wa Bukoba, Protas Mussa (38) mkazi wa Ngara, Kagera, Amos Skoth (38) makazi wa Mwanza,

Grace Rugambwa (67) mkazi a Bukoba na Amina Abdallah Karwandira (62) mkazi wa Bukoba.

Wengine ni Revina Theonest Rutinda (29) mkazi wa Geita, Emili Victor Mwesiga, Jesca Julius Titus (27) mkazi wa Dar es Salaam, Zang Lin (30) – Mchina, Richard Komba (42), Emmanuel Amani (28) mkazi wa Mwanza, Nikson Jackson Kawiche (35) mkazi wa Dar es Salaam, Saleh Omary (46), Edwin Bitegeko (33) mkazi wa Dar es Salaam, Eva Dickson Mcharo (38) mkazi wa Sengerema, Mwanza, Josephine Joseph Mwakisambwa (34)mkazi wa Dar es Salaam, Theodora Stanslays Mpesha (46) na oseph Laurence Mbago (57) mkazi wa Dar es Salaam.

Wahudumu walionusurika katika ajali hiyo ni wawili; Brenda Selvuli Temba (23) mkazi wa Dar es Salaam na Lydia Ibrahim Ramadhan (25) naye mkazi wa Dar es Salaam.

Waliofariki dunia watajwa

Abiria ambao wamepoteza maisha katika ajali hiyo ni pamoja na Atulinde Biteya, Aneth Biteya, Neema Faraja, Hanifa Hamza, Aneth Kaaya, Victor Laurean, Said Malat Lyangana, Iman Paul, Faraji Yusuph, Lin Zhang, Sauli Epimark, Zacharia Mlacha, Eunice Ndirangu, Mtani Njegere, Zaituni Shillah na Dkt. Alice Simwinga.

Rubani aliyepoteza maisha ni Buruani Rubaga na msaidizi wake Peter Odhiambo.

Majaliwa kuaga miili leo

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ambaye aliwasili mjini Bukoba jana jioni, na kutembelea manusura waliopelekwa hospitali ya Bukoba, leo anatarajia kuungana na Watanзания katika shughuli ya kuaga miili ya waliopeleza maisha katika ajali hiyo.

Shughuli za kuaga miili hiyo zitafanyika katika Uwanja wa Kaitaba na wananchi wameombwa kujitokeza kwa wingi kuaga marehemu.

Mwinyi kufuta chozi la Wazanzibar

Na Jabir IDRISSA, Zanzibar

AKIWA ametimiza miaka miwili Asasa tangu kuwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameongeza matumaini ya wanachi kwamba serikali yake itahakikisha inafuta chozi la umasikini ulio topea na kurejesha mali za walio dhulumiwa.

Dkt. Mwinyi aliipishwa kuwa kiongozi wa visiwa hivyo Novemba 2, 2020 baada ya kutangazwa mshindi katika uchaguzi uliofanyika mwaka huo. Alimshinda mpinzani wake mkubwa, Maalim Seif Shariff Hamad wa ACT-Wazalendo.

Rais Mwinyi ametoa uhakika huo juzi alipoulizwa swali na mmoja wa wahariri wa Pambazuko, aliyetaka kujua ni lini waliokuwa wateja wa Benki ya FBME watalipwa haki za amana zao baada ya benki kufungwa. Pia alitaka kujua hatma ya wafanyakazi wa waliokuwa watumishi kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA) uliopo Kisauni mjini hapa.

Amesema Wazanzibari kama ilivyo kwa wateja wengine wa Benki ya FBME, watalipwa haki zao kwani taratibu za kuhakikisha wanalipwa zinaendelea kwa Benki Kuu (BoT) na taasisi zingine kufanya upembuzi wa kina.

Rais Mwinyi amesema kisheria ni jukumu la BoT kushughulikia suala hilo la kulinda na kusimamia amana zilizowekwa inapotokea benki imepata matatizo na akaongeza kusema kuwa serikali inafuatilia kwa karibu kuhakikisha haki hizo hazipoteti.

FBME iliyokuwa na wanahisa kutoka Uarabuni, ilikuwa na matawi mawili nchini - moja jijini Dar es Salaam na Zanzibar. Huduma zilifungwa ghafla Mei 5, 2017 huku kukiwa na amana za mabilioni za Watanzania.

Hakujawa na taarifa ya kuwa FBME ilifilisika na tangu wakati huo hakujatolewa taarifa rasmi ya kilichotokea zaidi ya fununu kuwa benki ilifungwa ili kuridhia matakwa ya mataifa



Dkt. Hussein Ali Mwinyi

ya magharibi yaliyoamini ikitumika kufadhili shughuli za kigaidi.

Baadhi ya wenye amana FBME wameieleza Pambazuko kuwa hawajapewa maelezo ya kuridhisha kuhusu hatma ya fedha zao. "Tuliitwa mara moja na kuambiwa tutalipwa amana zetu, lakini hakuna maelezo yaliyonyooka wakati fedha tulizoweka tulikuwa na malengo ikiwemo kusaidia vijana wetu kujiendeleza kielimu," alieleza mmoja wao.

Kuhusu watumishi wa AAKIA, Rais Karume amekuwa akieleza kwamba stahiki zao hazitapotea na kwamba Kampuni ya DNATA iliyopewa kandarasi ya kuendesha uwanja wa AAKIA, utendaji wa kampuni hiyo utaongeza mapato maradufu kwani imedhihirika kufanya vyema katika viwanja vikubwa duniani, ikiwamo Dubai, Falme za Kiarabu.

Amesema serikali imeamua kutoa mkataba kwa DNATA kwa lengo la kuongeza mapato kupitia wageni mbalimbali wanaofika Zanzibar kwa shughuli za kitalii na za uwekezaji kwa kutumia eneo la uwanja mpya lilolojengwa kwa zaidi ya Dola 120 milioni.

Rais Samia avuna China

Rais Samia Suluhu Hassan akikagua gwaride aliloandaliwa wakati wa ziara yake China.


KATIKA kile kinachoweza kuelezwa kuwa ni kuhangaikia Watanzania, Rais Samia Suluhu Hassan hapumziki; yuko huku na kule kusaka “ugali wa watoto ” na Novemba 2, mwaka huu, alisafiri hadi China na kukutana na kiongozi wa nchi hiyo tajiri, Xi Jinping mjini Beijing.

Akiwa huko, Rais Samia na mwenyeji wake, walishuhudia kuwekwa kusaini mikataba mbalimbali ya ushirikiano ambayo wanadiplomasia wamesema itanufaisha kila upande.

Rais Samia anakuwa kiongozi wa kwanza kutoka Afrika kukutana na Jinping, hali ambayo inaelezwa kuwa ni “kuthamini” Tanzania na watu wake.

Mikataba iliyosainiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya usafiri - barabara, reli na bandari. Katika mikataba hiyo, China imetoa msaada wa Sh. bilioni 31.5.

Picha hizi za Ikulu ni matukio mbalimbali baada ya kuanza kwa ziara hiyo.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na mwenyeji wake, Rais Xi Jinping wa China jijini Beijing

Watumishi watano MDH wafariki

Na Mwandishi MAALUM

ABIRIA watano kati ya watu 19 waliofariki katika Ajali ya ndege ya shirika la ndege la Precision Air iliyotokea leo Novemba 6 Bukoba mkoani Kagera, ni watumishi wa Menejimenti na Maendeleo ya Afya (MDH).

Ajali hiyo imetokea leo Novemba 6 wakati ndege hiyo ikijaribu kutua katika uwanja wa ndege wa Bukoba, lakini kutokana hali ya hewa kuwa mbaya, ilipoteza mwelekeo na kutumbukia katika ziwa Victoria.

Mkurugenzi Mtendaji wa MDH, Dk David Sando amelithibitishia Mwananchi kuwa watumishi hao watano ni miongoni mwa wengine wanane wa ofisi hiyo waliokuwa safarini kwenda Bukoba.

“Watumishi wetu jumla walikuwa wanane na awali walitolewa watatu ambao hali zao hazikuwa nzuri

wakapelekwa hospitali lakini baadaye waliweza kutolewa watano ambao hawakuweza kuishi, wamefariki,” ameeleza Dk Sando kwa masikitiko.

Ametaja majina ya watumishi waliopoteza maisha kuwa ni pamoja na watafiti watatu wakiwemo Dk Boniface Jullu, Dk Neema Faraja na Dk Alice Simwinga pamoja na Sauli HappyMark pamoja na Mkuu wa kitengo cha mawasiliano MDH ZarchariaMlacha.

Amewataja watumishi watatu waliofanikiwa kuokolewa kuwa ni pamoja na Nickson Jackson, Dk Josephine Mwakisambwe na Dk Felix Otieno.

Dk Sando amesema wataalamu hao wa afya ya jamii walikuwa wakielekea Tabora wakipitia Mwanza na kwamba lengo la safari hiyo ilikuwa ni mkutano wa mwaka kwenda kuangalia maendeleo ya miradi.

Mwananchi



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akipewa maelezo na mkuu wa mkoa wa Kagera Albert Chalamila, baada ya kuwasili mkoani Kagera, Bukoba kufuatia ajali ya ndege ya Precision jana (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

Kuondoa darasa la saba ni upofu

Na Godwin CHILEWA,
Texas

MABADILIKO ni kitu cha kawaida, na tena cha lazima katika maisha. Yamkini pasipo mabadiliko hakuna mtu, jamii, wala nchi yoyote inayoweza kupiga hatua.

Mabadiliko ndiyo yanayofanya nchi ya wenye ufahamu kusonga mbele, na ile ya wasiojitambua kuachwa palepale au kurudishwa nyuma kwa kasi. Ni kwa sababu hii mataifa yaliyoendelea hufanya mabadiliko ya kila aina, na mara kwa mara katika mifumo yake ili kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Katika kufanikisha hilo mataifa yenye kujitambua hufanya kila liwezekanalo kuiga teknolojia mpya. Nchi kama China, Russia, India na nyinginezo hupenyeza maelfu ya raia zake nchini Marekani na Ulaya kujifunza elimu mpya na kuiba siri za maendeleo.

Raia hao huingia katika nchi hizo wakiwa wanafunzi wa kawaida katika vyuo vikuu, au wahamiaji wanaotafuta kazi katika viwanda na taasisi za uchunguzi (research) wanazozikusudia. Hawa wote huwa na lengo moja tu, kuiba siri za sayansi na teknolojia na kuzipeleka kwao.

Siyo hivyo tu, bali kila mwaka serikali ya Marekani hutumia mamilioni ya fedha kwa ajili ya mambo ya kiusalama, hususani kuwasaka majasusi wa kigeni wanaojipenyeza nchini humo kwa lengo la kuiba siri za biashara na uchumi, sayansi na teknolojia, na zile za ulinzi na usalama.

Hili huenda sambamba na kuwatafuta wakukuzi (hackers) wa nchi mbalimbali wanaojaribu kuingia ndani ya mifumo mbalimbali ya nchi hiyo. Haya yote husababishwa na kiu waliyonayo wenzetu katika kukuza na kulinda ufahamu wao wa sayansi na teknolojia.



Wasiri wa Elimu - Prof. Adolf Mkenda

Kwa ufupi wanajua thamani ya elimu, wanatafuta kwa bidii na kulinda hazina yao isichukuliwe hovyoy hovyoy tu.

Nimeyasema haya kwa sababu bado naendelea kujiuliza sisi – Watanzania tuna ugonjwa gani? Hivi hawa wataalam wetu waliotuletea hii sera mpya ya elimu nchini wameitoa wapi? wamechukua mfano wa nchi gani? Na wametumia vigezo gani? Nani aliyewaambia kwamba kufupisha elimu ya msingi kutoka madarasa saba hadi sita itasaidia kuboresha elimu?

Kama hayo madarasa saba yaliyokuwepo bado hayakutosha kuwasaidia wanafunzi wengi hasa wa vijijini kupata elimu bora, je madarasa sita yatawaokoa kweli? Kigezo gani kilichotumika kufanya uamuzi huu? Au ni kwa sababu wataendelea moja kwa moja tu hadi kidato cha nne?

Tena huu mpango wa kuondoa mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi utasaidiaje kuwafanya wanafunzi wasome kwa bidii? Utafiti gani ulioonesha mtihani wa darasa la nne utasaidia wanafunzi kujiandaa vyema kwa elimu ya juu kuliko wa darasa

Kuondoa darasa la saba ni upofu

la saba? Kama matokeo ya mthani wa taifa wa darasa la saba uliokuwa ukiheshimiwa kwa kulindwa na maofisa wa Idara ya Usalama wa Taifa, Polisi (na wajumbe wengine wote wa kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya) haukutosha kuwatikisa wanafunzi, wala kuishitua serikali kuwa elimu ya Tanzania ina matatizo makubwa; Je, mthani wa darasa la nne utasaidia kweli? Utamshitua nani? Tena ukizingatia mwanafunzi anaufanya akiwa bado mtoto zaidi?

Kwa maoni yangu, mtu aliyetoa pendekezo la kubadilisha sera ya elimu hakufanya uitafti wa kutosha, au maelezo yake hayakueleweka na wale waliolifanyia kazi suala hili. Au pengine wahusika wamechukua mfano wa nchi moja iliyofanikiwa bila kujua undani wa mfumo huo.

Nakumbuka hata Zanzibar walikuwa wana mfumo wa aina hii pia. Kwa kifupi, mfumo huu unafanana sana na ule unaotumika nchini Marekani na nchi nyingine zilizoendelea, Ni mfumo wenye gharama kubwa, na unafaa kwa nchi inayojiweza kiuchumi. Hauko rahisi kama wataalam wetu wanavyofikiri.

Kwa mfano, mwanafunzi wa Marekani huanza elimu ya awali (elementary education) darasa la chekechea (Kindergarten) na kuendelea hadi darasa la nne. Anapoingia darasa la tano hupelekwa shule ya kati (Middle School) ambapo husoma hadi darasa la nane. Hapo huwa ndiyo mwisho wa elimu ya awali, mtoto hupelekwa shule ya upili (High school) ambako husoma darasa la tisa hadi la kumi na mbili. Akimaliza (na kufaulu vyema) huenda moja kwa moja chuo kikuu.

Ukiangalia kijuujuu unaweza kudhani huu ni mfumo usio na maswali mengi, lakini sivyo. Katika kipindi chote mwanafunzi anapokuwa shuleni hufanyishwa mitihani mingi kupima uwezo wake. Baadhi ya mitihani hiyo



Wanafunzi wakiwa darasani

hutungwa katika shule anayosoma, na mingine huwa ya kiwilaya (School district) na kitaifa (State exams). Mwanafunzi anayeshindwa kufikia alama ya ufaulu iliyowekwa hulazimika kurudia darasa. Kwa mfano, katika jimbo la Texas wanafunzi hulazimika kufanya mitihani ifuatayo:

Mtihani wa Vipaji Maalum (Gifted Talented Students Test)

Mtihani huu ndiyo wa kwanza kabisa anaopeva mwanafunzi katika Jimbo la Texas. Mtoto hufanyishwa mthani huu (kupima IQ yake) akiwa shule ya chekechea (Kindergarten) au darasa la kwanza.

Huu ndiyo mthani unaoamua kama mtoto husika anafaa kuingizwa katika madarasa ya watoto wenye vipaji maalum (Gifted talented) au la. Mtoto akifaulu moja kwa moja huingizwa katika madarasa ya watoto wenye vipaji maalum ambayo utaratibu wake wa masomo ni tofauti. Kama akishindwa huwekwa

Kuondoa darasa la saba ni upofu

katika madarasa ya watoto wa kawaida.

Hata hivyo, wakati wowote ule (kati ya darasa la kwanza na la pili) mwalimu akimuona mtoto ana ufahamu usio wa kawaida hupendekeza afanyiwe mtihani huo. Mtoto aliyefaulu kuingia madarasa ya watoto wa vipaji maalum (GT), hutakiwa kuendelea kuonesha uwezo wake darasani kipindi chote anachokuwa shuleni; kama akionesha kutomudu madarasa ya vipaji maalum (GT) hurudishwa katika madarasa ya wanafunzi wa kawaida. Mtoto anayemalkiza elimu ya awali katika madarasa ya vipaji maalum hupelekwa Middle school na High school za watoto wa vipaji maalum.

Mitihani ya Wilaya (School District)

Kila mwaka wanafunzi wa shule ya awali (elementary school) hufanya mitihani wa wilaya (school district test). Mitihani huu hufanywa mara moja kwa mwaka, kutegemea ratiba ya wilaya husika. Lengo la mitihani hii ni kumhakikishia mzazi kuwa maendeleo ya mtoto wake ni mazuri au mabaya kama yanavyooneshwa katika taarifa (report card) ya matokeo ya majaribio na mitihani inayotungwa na mwalimu wa darasa lake.

Hii huondoa utata kuwa walimu wanawafundisha watoto majibu badala ya kuwafundisha waelewe. Pia huondoa malalamiko au hisia ya mzazi wa mtoto asiyefanya vyema darasani kuwa mwanawe anakatwa alama zake au hatendewi haki.

Mtihani wa Taifa (Texas STAAR Test).

Huu ni mitihani wa taifa (State Exam) unaofanywa kila mwaka na wanafunzi wa shule ya awali (Elementary school) na wale wa shule ya Kati (Middle School) kuanzia darasa la tatu (third grade) hadi darasa la nane (eighth grade).

Mtihani huu huhusisha masomo ya hesabu, sayansi, kusoma na kuandika. Mwanafunzi asiyefaulu mtihani huu

hulazimika kuurudia mara ya pili (wakati mwingine) asipofaulu tena hulazimika kurudia darasa.

Mitihani ya Mwisho (Final Exams)

Ili mwanafunzi atambulike kuwa amehitimu shule ya upili katika Texas Public High schools ni lazima afaulu masomo matano katika mtihani wake wa mwisho. Masomo hayo ni English - Reading, Mathematics (Algebra), Historia (U.S History), na English - Writing. Mwanafunzi asiyefaulu hutakiwa kurudia darasa.

Kama unavyoona huu siyo mfumo rahisi kama watengeneza sera wetu wanavyofikiria. Unahitaji maandalizi, usimamizi wa hali ya juu, na fedha nyingi za uendeshaji. Ni mfumo mzuri lakini una gharama isiyokwepeka.

Kwani ili uwe na wahitimu bora ni lazima wajaribiwe na kuthibitishwa kwa mitihani. Je, tuko tayari kubeba mzigo huo? Kama hatuna uwezo wa kufanya hivyo kwa nini tunataka kuchukua mfumo tusiouweza?

Huu tulionao tunashindwaje kuusimamia hadi uoneshe mafanikio? Je, tatizo ni sera au usimamizi? Je, hiyo sera mpya itaongeza uwezo wa walimu wetu kufundisha? Au utamfaidisha nani?

Kumbe ni vyema serikali iangalie upya marekebisho ya sera ya elimu kabla ya kukurupuka na utekelezaji wake.

Kitendo cha kuondoa mtihani wa darasda la saba ni dalili ya kutosha kuwa sera hiyo itawaathiri zaidi wanafunzi kimasomo. Mtihani huo licha ya kuwa kipimo cha uelewa wa mwanafunzi, ndiyo pia uliokuwa kigezo cha kuwepo kwa Qualifying Test (QT), mtihani uliokuwa ukifanywa na watu waliotaka kufanya mtihani wa taifa wa kidato cha nne kama watahiniwa binafsi. Kuondolewa kwa mtihani wa darasa la saba moja kwa moja kunafuta Qualifying Test (GT). Je wanafunzi binafsi watapimwaje?

Tusipoziba ufa tutajenga ukuta.

Hujambo

Wakati hutengeneza kitenzi ‘kuwa’

Na Dkt. Michael Mashauri

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo tutaendelea na somo linalohusu Kitenzi cha ‘kuwa’ (the verb ‘to be’) katika Kiswahili hujitokeza tofauti kulingana na wakati.

Wakati uliopo yakinifu hutumia **NI** na ukanushi wake ni **SI** katika umoja na wingi. (The verb ‘to be’ in Kiswahili appears in different forms according to the tenses. The present tense affirmative uses **NI** and negation is **SI** in singular and plural). Examples:

| | | |
|----------|-------------|--|
| Singular | Affirmative | Mimi ni mwalimu (I’m a teacher) |
| | Negative | Mimi si mwalimu (I am not a teacher) |
| Plural | Affirmative | Sisi ni wanafunzi bora (We are good students) |
| | Negative | Sisi si wanafunzi (We are not students) |
| Singular | Affirmative | Ugali ni mtamu sana (Ugali is so delicious) |
| | Negative | Kisu si kizuri (A knife is not good) |
| Plural | Affirmative | Viti ni vizuri (Chairs are good) |
| | Negative | Visu si vizuri (Knives are not good) |

Wakati mwingine wakati uliopo yakinifu hutumia viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli husika katika kuonyesha hai ya ‘kuwa’. Hata hivyo, kiambishi cha ukanushi hubaki kile kile. (Sometimes, the present tense affirmative uses subject concord (agreement prefixes) of respective noun class to show state of ‘being’. However, the negation remains the same.) *Examples:*

| | |
|----------|--|
| Singular | 1 st - Mimi ni mwalimu (I am a teacher) |
| | 2 nd - Wewe u mpole (You are polite) |
| | 3 rd - Yeye yu mwema (He/she is kind) |
| Plural | 1 st - Sisi tu wanafunzi (We are students) |
| | 2 nd - Nyinyi mu wema (You (all) are kind) |
| | 3 rd - Wao wa wakarimu (They are generous) |
| Singular | Mti u mrefu (A tree is tall) |
| Plural | Miti i mirefu (Trees are tall) |
| Singular | Tunda li kubwa (A fruit is big) |
| Plural | Matunda va makubwa (Fruits are big) |
| Singular | Kiazi ki kitamu sana (A potato is so delicious) |
| Plural | Viazi vi vitamu sana (Potatoes are so delicious) |
| Singular | Pikipiki i barabarani (A motorcycle is on the road) |
| Plural | Pikipiki zi ndani (Motorcycles are inside) |

• Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Urais wa Ruto bado watesa

Na Joseph WANGUI

FUKUTO la kutotambua uhalali ushindi wa Rais wa Kenya, Dkt. William Ruto bado linawasumbua wapinzani wake wakubwa.

Baada ya Mahakama ya Upeo ya Kenya kuthibitisha ushindi wa Ruto, bado alioshindana nao, wanatamani kusikia uamuzi tofauti kutoka vyombo vingine vya sheria.

Sasa kiongozi wa Chama cha NARC Kenya, Martha Karua anaelekeza nguvu zake katika Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki (EAC) akishutumu Mahakama ya Upeo nchini kwa kutupilia mbali kesi ya kupinga ushindi wa Ruto katika uchaguzi mkuu uliopita.

Karua katika shauri lake hilo, ameungana na Shirika la Kupigania Haki ya Waislamu Kenya (Muhuri), wakiishitaki Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka Kenya (IEBC) kwa madai ya kuvuruga uchaguzi huo wanaodai kuwa mshindi alikuwa anajulikana tayari – mpinzani wa Ruto, Raila Odinga.

Karua aliyekuwa mgombea-mwenza wa kinara wa Azimio la Umoja, Raila kwenye uchaguzi huo wa Agosti 9, mwaka huu alisisitiza kauli yake ya awali kuwa baadhi ya watu walivuruga mitambo ya IEBC na kubadilisha matokeo kwa manufaa ya Ruto.

Kiongozi huyo wa chama cha upinzani alishutumu Mahakama ya Upeo



Dkt. William Ruto



Martha Karua

akisema kuwa haikutenda haki baada ya kushindwa kuamrisha matokeo katika vituo vyote vya kupiga kura yahakikiwe.

Kati ya masuala yaliyoibuliwa na Karua dhidi ya korti hiyo ya upeo, inayoongozwa na Jaji Mkuu Martha Koome, ni uamuzi wake kuhusu masuala mbalimbali yenye utata kuzinzana na ule uchaguzi mkuu wa 2017 ambao ulichangia ushindi wa Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta kufutwa.

“Mahakama ya Upeo ilikataa kutumia sheria kuamua masuala tata kuhusu wajibu wa IEBC katika uchaguzi huo. Kulikuwa na wizi wa kura, ufisadi na mambo mengine ambayo yalitilia shaka uwazi katika uchaguzi huo,” inasema sehemu ya maombi ya kesi aliyowasilisha Karua.

Kesi hiyo imewasilishwa na mawakili Donald Omondi Deya na Esther Muigai-Mnaro na imejikita hasa katika jinsi ambavyo teknolojia ilivyoshindwa kufanikisha uchaguzi na pia mtambo wa IEBC kuvurugwa.

Karua anaitaka mahakama hiyo ya kikanda, iamue kuwa Mahakama ya Upeo haikufuata sheria kwa kuzingatia katiba na sheria za nchi.

Usawa sasa upambanue haki

Na Deusedith KAHANGWA

TANGU Azimio la Zanzibar lilipochukua nafasi ya Azimio la Arusha, sababu kuu ya kudai katiba mpya Tanzania ni hoja kwamba katiba ya sasa inatoa mwanya wa kukiukwa kwa “kanuni za mastahili ya kijamii” (principles of justice), kiasi cha kuwafanya baadhi ya raia kufikiri, kuhukumu na kutenda kama watumwa ndani ya nchi yao.

Hivyo, swali la pili kuhusu ‘ujasiriadola’ unaofanyika kupitia mchakato wa katiba mpya kwa ajili ya Tanzania mpya, linapaswa kuwa hili hapa:

“Kama tukichukulia kwamba jamii inayoheshimu “kanuni za stahili” za raia wake ni kikundi cha watu walio chini ya mamlaka moja wakishirikiana kufukuzia maslahi ya pamoja, ambapo maslahi hayo ni hatua ya kwanza katika safari ya kutafuta maslahi binafsi, ushirikiano huo unapaswa kuongozwa na “kanuni za stahili” zenye sura gani?”

Profesa John Rawls (1921-2002) wa Marekani. alijibu swali hili baada ya kuchukua mazuri ya nadharia za stahili (theories of justice) zinazofahamika, na kutupilia mbali upungufu wake.

Nadharia hizo ni pamoja na: ubepari, ujamaa, ulibatariani, uegalitariani, uperisona, uyutilitariani, kanuni ya dhahabu kwa mujibu wa misahafu, na kadhhalika.

Kwa mujibu wa jawabu la Rawls, dola ambayo ni “jamii yenye kujali kanuni za stahili inasimamia mgawanyo wa haki na majukumu miongoni mwa wanajamii kwa kuzingatia kaulimbiu ya “kuongeza usawa na kupunguza utofauti” katika jamii. Rawls anaitafsiri kaulimbiu hii kwa njia ya kanuni kadhaa.

Mosi, Rawls anaongelea kanuni ya uhuru sawa kwa raia wote. Kwa mujibu



Profesa John Rawls

wa kanuni hii, kila mtu anayo haki sawa kuhusu uhuru wa msingi, uhuru ambao kila binadamu anao kwa usawa.

Kanuni hii inasema kwamba, uhuru wa kila raia unapaswa kulindwa dhidi ya mashambulizi kutoka kwa watu baki.

Hapa kuna uhuru wa kuishi, kufikiri, dhamiri, kuabudu, kupiga kura, kujieleza, kusambaza habari kupitia vyombo vya habari, kutafuta na kumiliki mali binafsi, kukusanyika, kwenda popote bila kuvunja sheria, kutokamatwa kiholela, uhuru wa faragha, uhuru dhidi ya rushwa za uchaguzi, na uhuru dhidi ya ulaghai katika mikataba na matangazo.

Pili, Rawls anaongelea kanuni ya kupunguza makorongo kwenye uwanja wa kisiasa. Kwa mujibu wa kanuni hii, tofauti za kisiasa zinapaswa kupunguzwa kwa kuhakikisha kwamba, mazingira yaliyopo yanajenga uwanja ulio tamarara kwa ajili ya watu wote wanaotaka kugombea nafasi za kiofi katika taasisi za kijamii.

Tupunguze pengo kati ya matajiri na masikini

Kwa mujibu wa kanuni ya uhuru sawa kwa wote, pamoja na kuwa, nafasi za uongozi ni chache kuliko wananchi, bado

Usawa sasa upambanue haki

Inatoka Uk. 21

yanapaswa kujengwa mazingira ambayo yanaondoa ubaguzi holela kwa sababu ya tofauti kama vile rangi, kabila, ukoo, jinsi, dini, eneo la kijiografia anakotoka mtu, na uwezo wa kifedha.

Kwa sababu hii, Rawls anapendekeza kwamba, wakati wa uchaguzi, serikali inapaswa kugharimia kampeni za wagombea wote, kama njia mojawapo ya kujenga uwanja tambarare kwa wagombewa hawa.

Tatu, Rawls anaongelea kanuni ya kupunguza pengo la kiuchumi. Kanuni hii inatamka kuwa, tofauti za kiuchumi zinapaswa kupangiliwa katika namna ambayo inazalisha manufaa makubwa kwa watu wanyonge katika jamii.

Kwa mujibu wa kanuni hii, pamoja na kwamba, mfumo wa kiuchumi unaambatana na tofauti za ujuzi, stadi, kipato, na mali, lakini bado jamii lazima ichukue hatu za makusudi za kuwainua watu wanyonge katika jamii, wakiwemo wagonjwa, walemavu, wazee, watoto, na makundi ya watu yasiyo na nyenzo za uzalishaji.

Kanuni hii inataka watu wenye ujuzi fulani wafanye kazi zinazohusiana na ujuzi huo, bila kujali tofauti holela kama vile za rangi, jinsi, dini, kabila, au eneo la kijiografia.

Pia, kanuni hii inataka kila mtu apate elimu na mafunzo, bila ubaguzi unaotokana na uwezo wa kulipia, ili kwa njia hiyo, watu wote wapate sifa ya kuajiriwa katika kazi na kujipatia mkate wao wa kila siku kutokana na juhudi na maarifa binafsi.

Kwa hiyo, kanuni hii inahimiza kanuni za soko huria katika ajira na uzalishaji; inahimiza uwepo wa serikali inayotoza kodi na kuitumia kodi hiyo katika kujenga usawa kwa kutoa huduma za kijamii zinazowanufaisha watu wanyonge.



Huduma hizo ni pamoja na elimu bure hadi chuo kikuu, huduma za afya; miundombinu ya barabara, maji, nishati, na tehamu; vyombo vya ulinzi na usalama; na maslahi ya pamoja kama haya.

Chini ya kanuni hii, Rawls anateta “kanuni za stahili” na anazigawa katika makundi manne.

Mosi, kuna “kanuni za stahili” katika mauziano kwa mujibu wa mkataba, yaani “commutative justice.”

Pili, kuna “kanuni za stahili” katika kuchangia keki ya taifa kwa kufanya kazi na kulipa kodi stahiki serikalini, yaani “contributive justice.”

Tatu, kuna “kanuni za mastahili” katika kugawanya keki ya taifa kupitia huduma za jamii ili kupunguza pengo la maisha kati ya matajiri na maskini, yaani “redistributive justice.”

Nne, kuna “kanuni za stahili” katika malipo ya fidia stahiki kwa mtu aliyefanyiwa uonevu na watu, yaani “compensatory justice.”

Na tano, kuna “kanuni za stahili” katika kutoa adhabu inayolingana na uonevu alioufanya mtu dhidi ya wenzake, yaani “retributive justice.”

Wakomalia Hersi aombe radhi

Na Shaaban LULELA

MASHABIKI na baadhi ya wanachama wa mabingwa wa soka Tanzania, Yanga kutoka maeneo mbalimbali ya nchi, wameendelea kumtaka rais wa klabu hiyo, Hersi Said, kuomba radhi.

Wanahimiza kwamba kiongozi huyo amedharau idadi kubwa ya mashabiki wa Yanga kwa kauli yake kwamba; “watu wameshakula mihogo huko wanasema wameumizwa na matokeo.”

Hersi alitoa kauli hii alipokuwa akizungumza na viongozi wa matawi ya Yanga mkoani Mwanza wiki iliyopita kufuatia matokeo ya suluhu yaliyoonekana kutowaridhisha mashabiki hao dhidi ya timu ya Club Africain ya Tunisia kwenye mchezo wa mkondo wa awali hatua ya mtoano Kombe la Shirikisho Afrika.

Tangu umma kufikiwa na kauli hiyo, mitandao ya kijamii imejaa kauli na maandishi yanayomtaka Hersi kuomba radhi kwa namna ambayo mashabiki wanaeleza “alizingumza kwa dharau ya hali ya juu akimaanisha mashabiki wanaolalama ni wenye maisha mavovu.”

Mihogo ni zao lenye faida kubwa kwenye mwili wa binadamu likiwa limesheheni wanga, madini ya chuma, lakini kwa baadhi ya jamii za Tanzania huonekana kama chakula dhalihi na hugeuka kuwa na thamani wakati wa njaa pekee.

Pamoja na wengi kumtaka kuomba radhi, wapo pia wanachama na mashabiki wanaomtetea Hersi wakieleza kwamba “huenda hakuwa na maana ya kejeli, bali msisitizo wa namna mashabiki walivyoumizwa na matokeo hayo.”

Khamis Maulid wa Kinondoni Mkwajuni, Dar es Salaam ameliambia Pambazuko kwamba Rais wa Yanga, hakuwa na makosa, alitumia tu lugha ya picha kusisitiza jambo na namna alivyokerwa timu yake kushindwa kuibuka na ushindi dhidi ya wapinzani wao.

“Hersi alikerwa kama ambavyo



Hersi Said

mashabiki wengine walichukizwa na matokeo, lakini waliowasilisha ujumbe kwa jamii, walikata kipande kidogo cha video na hapo ikaonekana anatoa lugha isiyopendeza kwa wengi,” ameingeza mwanachama huyo.

Akizungumzia kauli yake baada ya kuwa imeleta sintofahamu, Hersi amesema watu wasioitakia mema klabu ya Yanga wamekuwa wakitumia vibaya sehemu ya video za mkutano wake na wanachama wa Mwanza kwa lengo la kuchinganisha.

“Wapo baadhi ya watu wanataka kuona Yanga inavurugikiwa, hawa hawaitakii mema klabu yetu, wametumia vibaya sehemu ya kauli yangu ambayo nilitumia wakati nazungumza na viongozi wa matawi mkoani Mwanza wakieleza kuwa ni kama kuwakejeli mashabiki wa timu yetu, kitu ambacho siyo kweli,” ameingeza Hersi.

Hersi amewahakikishia wanachama kwamba uongozi wao ni sikivu sana, na kwamba umekuwa karibu sana na wanachama wa kila aina, na ndiyo maana umekuwa ukivatembelea na kuwafikia walipo bila ubaguzi wa aina yeyote.

PICHA KUBWA



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akimpa pole Levina Lutinda na Mwanaye Emmily Victor ambao wamenusurika katika ajali ya ndege ya Precision iliyotokea jana mjini Bukoba. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

